



KIJARIDA KUHUSU
DHAMANA

Kwa Jamii yenyeye Haki na Usawa





**Unaweza kutoa taarifa
za ukiukwaji wa haki
kupitia**

#HakiKiganjani



0699695486



Pakua AnroidApp
ya **Haki Kiganjani**



hakikiganjani.humanrights.or.tz

Usipotezee, toa taarifa sasa!



KIJARIDA KUHUSU
DHAMANA

Kimeandaliwa na:

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

YALIYOMO

1.	DHAMANA	11
1.1.	Maana ya Dhamana	11
1.2.	Misingi ya Dhamana	11
1.3.	Dhamana ni Haki na Sio Upendeleo	13
2.	MAMLAKA NA MAUDHUI YA DHAMANA	15
2.1.	Vyombo Vyenye Mamlaka ya Kutoa Dhamana.....	15
2.1.1.	Dhamana ya Polisi.....	16
2.1.4.	Dhamana ya Mahakama.....	17
2.2.	Sababu za Kuwaweka Rumande Watuhumiwa ...	18
2.2.1.	Urahisi wa Kumpata mtuhumiwa.....	18
2.2.2.	Kuiepusha Jamii na Madhara ya Jinai ya Mtuhumiwa	19
2.2.3.	Kuepusha Uvurugaji wa Ushahidi au Upelelezi ..	20
2.2.4.	Kulinda na Kuhifadhi Maisha ya Mtuhumiwa	20
2.3.	Makosa yanayoweza Kuwekewa Dhamana na yasiyoweza Kuwekewa Dhamana.....	20
3.	Aina za dhamana	23
3.1.	Dhamana ya Mkataba wa Maandishi	23
3.2.	Dhamana ya Utambulisho	23
3.3.	Kuomba Dhamana kwa Kuweka Fedha	24
3.4.	Dhamana ya Mali	25
4.	TARATIBU ZA KUOMBA DHAMANA.....	26
4.1.	Mtu Anayeruhusiwa Kisheria Kuomba Dhamana	26
4.2.	Wakati/Muda wa Kuomba Dhamana.....	27
4.3.	Kukubali Kosa na Athari Zake Kwenye Dhamana	27
4.4.	Kupewa Dhamana	28
4.5.	Mambo ya Kufanya Pale Maombi Dhamana Yanapokataliwa	28
5.	VIKWAZO NA MASHARTI YA DHAMANA	30
5.1.	Vipingamizi vya Dhamana	30
5.7.	Masharti ya Dhamana.....	32

SHUKRANI

Tunatoa shukrani kwa wanasheria wetu na wale wa kujitolea katika uandaaji wa vijarida hivi. Pia tunawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwenye kukirejea kijitabu hiki ili kuandaa toleo hili la nne hususani, Wakili Joanitha Mutayoba, Wakili Theresia Kinabo, Wakili Godfrey Mpandikizi, Bi Irene Nambuo na Bw. Rodrick Maro, pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya Watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi

kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama angejua sheria. Ndiyo maana basi Kituo kimeamua kutoa chapisho hili na mengine, kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi wa kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika kijitabu hiki tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia.

Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali umsaidie na mwenzako apate usaidizi huu.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania mnamo mwezi Septemba, mwaka 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam na Arusha kuna ofisi ndogo.

MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenyehaki na usawa.

TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibashara linalojibidiisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa unakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa kisheria.

UTANGULIZI

Imekuwepo hali fulani katika jamii ya watu wengi kutokufahamu maana ya dhamana, hutolewa kwa nani, nani ana uwezo wa kuitoa, ni vigezo gani hutumika kabla ya kutolewa na ina masharti gani.

Hali hii imefanya baadhi ya watu kutoa tafsiri mbalimbali tofauti kuhusu utoaji wake na katika mazingira fulani fulani utoaji wake umetafsiriwa vingine na kuzaa hisia mbaya dhidi ya mamlaka inayohusika na utoaji wake.

Fikra au hali hiyo imechangia kuongezeka kwa matukio ya kikatili ya kuwapiga, kuwachoma moto au kuwaua watuhumiwa wa makosa ya jinai hata kuwaua bila kuwfikisha kwenye vyombo vyya sheria. Wananchi wamekuwa wakitoa sababu kwamba wamechoka na tabia ya kuwaona watuhumiwa wakiachiwa bila ya maelezo ya kutosha muda si mrefu baada ya kufikishwa polisi. Hii inatokana na hisia kuwa, rushwa hutolewa hivyo watuhumiwa huachiwa.

Malalamiko mengine yenyewe uhusiano na dhamana yamekuwa yakinolewa mara nyingi katika jamii na mara nyingi matokeo yake yamekuwa ni watu kukosa haki zao na kunyanyasika.

Kutokana na wengi kutokuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu dhamana, mara nyingi huchukuliwa kuwa mfumo wa utoaji haki hauzingatii maslahi ya wananchi. Lengo la kijitabu hiki ni kutoa mwanga kwa msomaji kuhusu inachosema sheria juu ya dhamana pamoja na uhusiano wake na haki za binadamu ili aweze kutumia ufahamu huo pale hitaji linapojitokeza. Vilevile mwanga huo utasaidia kuondoa dhana ya kuwa kila mtuhumiwa mwenye kesi ya jinai ni lazima akae mahabusu kama wengi wanavyofikiri.

1. DHAMANA

1.1. Maana ya Dhamana

Wataalamu mbalimbali wa sheria wametoa tafsiri kadha wa kadha kuhusu maana ya dhamana. Kutokana na tafsiri hizo na matumizi ya kijitabu hiki dhamana inamaanisha uhuru wenye masharti apewao mtuhumiwa au mshtakiwa wakati shauri lake likiendelea kupelelezwa, likiendelea kusikilizwa mahakamani au likisubiri matokeo ya rufaa yake.

1.2. Misingi ya Dhamana

Katiba ya nchi yetu inaeleza wazi kuwa kila mtu anastahili kuwa huru kwani binadamu wote wamezaliwa huru na wote ni sawa. Katika nchi inayoongozwa na kuheshimu utawala wa sheria kuna ile dhana ya kuamini kwamba kila mtu hana kosa hadi hapo atakapothibitishwa na mahakama kuwa ni mhafifu. Hii hali ya kuonekana kutokuwa na makosa mbele ya sheria inaleta msingi mwengine wa

haki za asili za kimsingi ambazo zinasema mtu asihukumiwe bila ya kusikilizwa.

Vile vile kila mtu anastahili kutambuliwa na kuheshimiwa utu wake. Kwa kutambua kanuni hizi za msingi Katiba imeendelea kusisitiza ya kuwa ili kuhakikisha watu wote wako sawa mbele ya sheria, mamlaka ya serekali inapaswa kuweka taratibu nzuri na ambazo zitazingatia kuwa mtu yejote anayeshtakiwa kwa kosa la jinai hapaswi kufanyiwa kama vile ameshatiwa hatiani kwa kosa aliloshtakiwa nalo.

KUMBUKA:

Ibara ya 13(6)(b) ya Katiba inasema kuwa: Ni marufuku kwa mtu aliyeshtakiwa kwa kosa la jinai kutendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka itakapothhibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo.

Maelezo haya ya Katiba yana maana kwamba, mshtakiwa atatendewa kama mtu asiye na hatia hadi pale mahakama itakapothibitisha kosa lake. Ili kukazia msimamo huu, sheria inatoa msingi kuwa mtu asiadhibiwe kabla hajapewa haki ya kusikilizwa utetezi wake. Kwa hali hiyo, kuwepo kwa utoaji wa dhamana kwa mshtakiwa ni kuendelea kuheshimu haki yake ya kuwa huru hadi atiwe hatiani kwa kosa analoshtakiwa nalo. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai imefafanua taratibu zote za utoaji wa dhamana na masharti yake.

1.3. Dhamana ni Haki na Sio Upendeleo

Kwa kuwa dhamana ni haki ya mtu, hivyo anapoomba hapaswi kukataliwa bila sababu za msingi. Mahakamani na wanaharakati wa haki za binadamu wamesisitiza mara nyingi kuwa dhamana ni haki ya mshtakiwa pale anapotimiza masharti yake; kumnyima bila sababu ni kumkosesha haki ya msingi ya kuwa huru kwa mujibu wa sheria. Vile vile polisi au

mahakama inapokataa kutoa dhamana ni lazima kuwe na sababu nzito zenyе kuridhisha kabla ya kufikia uamuzi huo.

Hapa Tanzania sheria imeweke wazi kuwa ni kesi za mauaji, wizi wa kutumia silaha, uhaini, kuhujumu uchumi na utakatishaji fedha tu ambazo kutohana na uzito wake mtuhumiwa hawezi kuwekewa dhamana ila kesi nyingine zote zilizobaki, mshtakiwa anayo haki ya kuwekewa dhamana, pindi akitimiza masharti ya dhamana na mahakama ikaridhika. Kwa msingi huu dhamana ni haki ya mshtakiwa na kupewa dhamana ni katika kutimiza haki hiyo ya msingi.

Mahakama inaweza kukataa kutoa dhamana iwapo itakuwa imeridhika kuwa kutolewa kwa dhamana kutaharibu maana nzima ya kesi hiyo kuwepo mahakamani, kutavuruga kesi hiyo, au mshtakiwa anaweza kupata madhara ikiwa ataruhusiwa kurudi kwenye

jamii. Na wakati mwingine dhamana inaweza kukataliwa pale itakapoonekana mtuhumiwa anaweza kutoroka.

ANGALIZO:

Hali hii ndiyo inayosababisha kesi za mauaji na uhaini kukataliwa dhamana kwani adhabu yake ni nzito (kifo) ambapo ni rahisi mshtakiwa kushawishika kutoroka.

2. MAMLAKA NA MAUDHUI YA DHAMANA

2.1. Vyombo Vyenie Mamlaka ya Kutoa Dhamana

Kutoa dhamana ni wajibu wa kisheria ambao unapaswa kufanywa kwa kuzingatia misingi na kanuni za sheria kwa hali hiyo siyo kila mamlaka inaweza kutoa dhamana. Mamlaka zinazoweza kutoa dhamana ni Polisi na Mahakama.

2.1.1. Dhamana ya Polisi

Kwa ujumla kuna dhamana zitolewazo na Polisi na kuna zile zitolewazo na Mahakama. Dhamana ya polisi hutolewa kwa mtuhumiwa aliyeko chini ya ulinzi na mkuu wa kituo cha polisi ambapo mtuhumiwa anashikiliwa na bado hajapelekwa mahakamani. Kwa ujumla Polisi wanapaswa kumwachia mtuhumiwa baada ya kujidhamini mwenyewe kwa maandishi au kudhaminiwa na wadhamini wanaoaminika ikiwa: mtuhumiwa alikamatwa pasipo hati ya kumkamata mshtakiwa; au ikiwa baada ya upelelezi imebainika kuwa hakuna ushahidi wa kutosha; au ikiwa mashtaka yake siyo ya makosa makubwa; au ikionekana kuwa upelelezi wa ziada unahitajika na kwamba hauwezi kukamilika ndani ya saa ishirini na nne (24) tangu kukamatwa kwa mtuhumiwa.

Muhimu:

1. Ikiwa mshtakiwa ni mtoto mwenye umri chini ya miaka kumi na tano lazima aachiliwe mara mzazi au mlezi au ndugu au mtu yejote mwenye kuaminika atakapomuwekea dhamana;
2. Ni marufuku kwa afisa wa polisi kupokea fedha kama ada ya dhamana, au malipo yoyote kwa ajili ya kuendesha kesi, kutoa ushahidi, au kumkamata mtuhumiwa;
3. Mtuhumiwa ana haki ya kupewa taarifa kamili kuhusu sababu za kukamatwa kwake, na haki ya kupata dhamana kwa mujibu wa sheria, na ikiwa Polisi atakataa kutoa dhamana kwa mtuhumiwa, ni lazima Polisi huyo abainishe kwa maandishi sababu za kukataa kwake.

2.1.4. Dhamana ya Mahakama

Dhamana ya Mahakama ni dhamana inayotolewa na mahakama baada ya mshtakiwa kusomewa mashtaka yake na kukana kosa. Kisheria dhamana hii ina

lengo la kumruhusu mtuhumiwa kuwa nje ya mahabusu hadi pale mahakama itakapotoahukumu.Dhamanahiihuweza kutolewa na Jaji au Hakimu. Mahakama Kuu ya Tanzania ndiyo iliyio na uwezo wa mwisho wa kuamua kutoa dhamana au kutokutoa kwa yale makosa ambayo sheria inaruhusu dhamana. Kwa hali hiyo madhumuni ya dhamana ni kwamba hata kama mtu ameshtakiwa kwa kosa la jinai bado ana haki zake zote za kimsingi kwani bado hajathibika kisheria kutenda kosa hilo. Kwa kusema kuwa dhamana ni haki ya mshtakiwa ina maana kuwa pale mshtakiwa anaposhitakiwa anayo haki ya kuwekewa dhamana ila kuna mazingira yanayoweza kusababisha mshtakiwa asipewe dhamana.

2.2. Sababu za Kuwaweka Rumande

Watuhumiwa

2.2.1. Urahisi wa Kumpata mtuhumiwa

Lengo la kumweka mshtakiwa rumande ni kuhakikisha kwamba siku ya kesi

anapatikana na kuwepo Mahakamani kujibushtaka au mashtakanayomkabili pindi atakiwapo kufanya hivyo.

Kwa hiyo, Mahakama ikiridhika kwamba mshtakiwa atafika Mahakamani kujibu shtaka pale atakapohitajika, basi Mahakama katika hali hiyo ina uwezo wa kumpa mshtakiwa dhamana.

2.2.2. Kuiepusha Jamii na Madhara ya Jinai ya Mtuhumiwa

Pale ambapo haki za mshtakiwa zitagongana kuashiria madhara na taathira kwa haki za msingi za jamii inayomzunguka mshtakiwa anaweza kunyimwa dhamana. Hivyo basi mahakama inaweza kuamuru mtuhumiwa awekwe rumande ili asiendeleze madhara dhidi ya jamii inayomzunguka. Hata hivyo uamuzi wa mahakama kumnyima au kumpa dhamana mtuhumiwa unapaswa kuwa na sababu za kimsingi.

2.2.3. Kuepusha Uvurugaji wa Ushahidi au Upelelezi

Wakati mwingine, mtuhumiwa hulazimika kuwekwa rumande ili kusaidia upelelezi kuendelea bila kuingiliwa au ushahidi kuvurugwa. Mara nyingi sababu hii hutegemea sana aina na mazingira ya jinai iliyotendwa na mtuhumiwa.

2.2.4. Kulinda na Kuhifadhi Maisha ya Mtuhumiwa

Mwisho, mtuhumiwa anaweza kuwekwa rumande ikiwa makosa aliyotenda yatasababisha au yataamsha chuki kubwa na uchu wa kulipiza kisasi toka kwa wanajamii. Katika hali hiyo mahakama huweza kutumia uwezo wake kumnyima mshtakiwa hiyo dhamana na kuamuru akae rumande ili kunusuru maisha yake.

2.3. Makosa yanayoweza Kuwekewa Dhamana na yasiyoweza Kuwekewa Dhamana

Sheria za Tanzania zime wekawazi makosa ambayo mtu akituhumiwa kuyatenda

hatakuwa na haki ya kupata dhamana na makosa ambayo mtuhumiwa anastahili dhamana. Wakati mwingine hutokea mtuhumiwa kunyimwa dhamana na Mahakama za chini lakini ikiwa mtuhumiwa huyo ana haki kisheria basi anawezakukatarufaakwenda Mahakama Kuu na ikaridhia kumpatia dhamana ikiwa shitaka lake linaruhusu dhamana. Hivyo suala la kupewa dhamana na kutokupewa linategemeana na masharti ya dhamana, ngazi ya mahakama husika na aina ya kosa.

Kuna ugumu kisheria wa kutoa dhamana ikiwa mshtakiwa anatuhumiwa kwa makosa makubwa. Hayo ni makosa ambayo adhabu zake ni kifo au kifungo cha maisha. Uzito huu wa adhabu umekuwa kitisho kwa watuhumiwa na hivyo husababisha washtakiwa kutoroka ili kuikwepa adhabu. Hili limeifanya Mahakama kuwa makini

zaidi na kujihakikisha kuwa washtakiwa wanafika Mahakamani. Njia pekee ya kufanikisha uhakika wa mtuhumiwa wa makosa makubwa kufika mahakamani imeonekana ni kumuweka rumande mshtakiwailiawezekukifika mahakamani kwa urahisi kuendelea na kesi.

Baadhi ya Makosa ambayo hayana dhamana kwa mujibu wa sheria za nchi ni kama vile:

- + Makosa ya mauaji;
- + Makosa ya wizi wa kutumia silaha;
- + Makosa ya utakatishaji fedha;
- + Makosa ya madawa ya kulevyा;
- + Makosa ya uhaini; na
- + Makosa ya kuhujumu uchumi

3. AINA ZA DHAMANA

Kuna aina mbali mbali za dhamana kama zifuatazo:

3.1. Dhamana ya Mkataba wa Maandishi

Huu ni mkataba wa maandishi anaoandikiana mshtakiwa au mdhamini na mahakama na itakapotokea kuwa mshtakiwa atashindwa kuhudhuria mahakamani katika siku iliyopangwa mdhamini atapaswa kutimiza masharti fulani fulani ambayo yatakuwa yameelezwa kwenye mkataba.

Mara nyingi sharti linalopaswa kutekelezwa ni mdhamini kutoa kiasi fulanicha fedha. Hii nia hadiatakayokuwa ameitoa katika mkataba huo.

3.2. Dhamana ya Utambulisho

Hii nia ina ya dhamana ambayo inafanana na ile ya mkataba wa dhamana, ila katika dhamana hii ni mtu mmoja tu ndiye anayetakiwa kuweka sahihi yake. Kama sahihi itawekwa na mshtakiwa, mdhamini hana haja tena ya kuweka

sahihi yake, vivyo hivyo kwa mdhamini. Dhamana ya aina hii inaelezea ahadi ya kulipa ambapo mara nyingi, malipo hayo hufuata baada ya kushidwa kutekeleza masharti fulani yaliyowekwa.

Kwa hiyo aina hii ya dhamana ni ahadi ya kulipa, ni wajibu wa kulipa unaoibuka baadaye pale mashartifulaniyalioelezwa ndani ya mkataba huu yanapokuwa hayajatimizwa. Masharti ya aina hii ya dhamana ni mepesi zaidi kuliko yale ya mkataba wa maandishi.

3.3. Kuomba Dhamana kwa Kuweka Fedha

Hii ni aina ya dhamana ambayo mshtakiwa, ndugu au rafiki huweka kiasi fulani cha fedha mahakamani. Hivyo mahakama badala ya kumtaka mshtakiwa aingie kwenye mkataba, huwa inaamuru mshtakiwa aweke kiasi fulani cha fedha, na kutoa ahadi kuwa kama mshtakiwa hataonekana siku ya kusikilizwa kesi, fedha hizo zitachukuliwa na serikali

Pamoja na kuwa mtu yeote anaweza kutoa fedha mahakama inaweza kuagiza kuwa fedha hizo zitolewe na mshtakiwa mwenyewe na inapaswa kufanywa hivyo. Mara nyingi aina hii ya dhamana huitwa dhamana ya fedha taslimu.

3.4. Dhamana ya Mali

Kama mshtakiwa hana fedha, mahakama itamtaka awekevitu kama dhamanayake. Hii dhamana inawasaidia wale ambao hawana fedha ilawanavitu vyenyethamani kuviweka vitu hivyo kama dhamana. Vitu au vifaa vitakavyowekwa ni vile ambavyo mshtakiwa anavimiliki au vinamilikiwa na mdhamini wakati anaomba dhamana, viwe ni vitu visivyohamishika. Vitu kama pasi ya kusafiria, leseni za udereva, hati za nyumba n.k huweza kuwekwa kama dhamana ingawa si mara nyingi sana kwani mshtakiwa anapokiuka masharti unatokea ugumu wa kutaifisha vitu hivyo. Iwapo vitu vya thamani vinawekwa kama dhamana thamani yake inapaswa kueleweka katika maandishi.

4. TARATIBU ZA KUOMBA DHAMANA

4.1. Mtu Anayeruhusiwa Kisheria Kuomba Dhamana

Dhamana inaweza kuombwa na mtuhumiwa mwenyewe au wadhamini wake. Kama dhamana itaombwa wakati mshtakiwa amekwisha hukumiwa [yaani wakati rufaa imewasilishwa] ni lazima iombwe na mtu mwengine, yaani wakili wa mshtakiwa au mtu mwengine.

Hivyo kama mshtakiwa yupo rumande mtu mwengine yeote yule anaweza kumwombea dhamana. Hakuna njia maalum ya kuomba dhamana bali itatosha tu pale mshtakiwa au wakili wa mshtakiwa atakaposema kuwa anaomba mshtakiwa apewe dhamana. Siyo lazima mshtakiwa awepo wakati wa kuomba dhamana ila kama anayeomba ni mshtakiwa, basi lazima awepo wakati wa kuomba dhamana

4.2. Wakati/Muda wa Kuomba Dhamana

Dhamana inaweza kuombwa wakati shtaka linatengenezwa au muda wowote kabla ya hukumu kutolewa. Kabla ya kuomba dhamana lazima kwanza kuwepo na mashtaka ya kusikilizwa.

Ni haki ya mshtakiwa kupewa hati ya mashtaka kwani husaidia kumfahamisha mshtakiwa anashtakiwa kwa kosa gani na vilevile hufafanua kwa undani kosa anapohitaji kuomba dhamana.

Mara nydingi baada ya mshtakiwa kusomewa shtaka na kujibu, kabla ya kuahirisha kesi hakimu humtamkia mshtakiwa kuwa dhamana ipo wazi na masharti ya dhamana ni yapi.

4.3. Kukubali Kosa na Athari Zake Kwenye Dhamana

Kama mshtakiwa baada ya kusomewa hati ya mashtaka anakiri kutenda kosa, dhamana inaweza pia kutolewa katika kipindi cha kukiri kutenda kosa na kutiwa hatiani au kuachiwa. Kama mshtakiwa

anang'ang'ania kukiri kosa mahakama inamhukumu moja kwa moja na suala la dhamana halitakuwepo tena hata baada ya kufafanuliwa kwa kina kosa lenyewe.

4.4. Kupewa Dhamana

Dhamana inaweza ikatolewa na Mahakama au Mkuu wa Kituo cha Polisi mtuhumiwa alipowekwa. Hii itatokea baada ya Hakimu/Jaji au mkuu wa kituo cha polisi kujiuliza maswali kadhaa iwapo atampa mshtakiwa dhamana kama vile; Je! Mshtakiwa atahudhuria kesi yake mahakamani au la, Je, mtuhumiwa ana historia ya kukimbia dhamana? Je, mtuhumiwa alishatenda tena kosa kama analotuhumiwa nalo? Uamuzi wa kutokutoa dhamana utoke kwa Hakimu/Jaji au Mkuu wa Kituo cha Polisi mwenyewe na siyo vinginevyo.

4.5. Mambo ya Kufanya Pale Maombi

Dhamana Yanapokataliwa

Kama mtu hatapewa dhamana katika mahakama za chini mshtakiwa itabidi

awasilishe maombi ya dhamana Mahakama Kuu. Hii ni kwa sababu Mahakama za chini na Mahakama Kuu zinatofautiana kingazi lakini zina uwezo sawa katika suala la dhamana

Maombi ya dhamana Mahakama Kuu siyo rufaa, ila ni maombi yanayotokana na kukataa kwa mahakama ya chini kutoa dhamana au kuweka dhamana yenye masharti magumu. Kwa hiyo atakachokuwa anafanya mshtakiwa ni kuandaa upya maombi ya dhamana na kuyapeleka Mahakama Kuu na siyo kukata rufaa.

Maombi kama haya hupelekwa Mahakama Kuu kwani ndio yenye uwezo wa kubadili maamuzi ya Mahakama za chini au hutoa dhamana pale Mahakama za chini zitakapokuwa zimekataa kutoa.

5. VIKWAZO NA MASHARTI YA DHAMANA

Dhamana ni haki ambayo upatikanaji wake unategemeana na jinsi mshtakiwa alivyofuatataribuna mashartiyaliyowekwa na sheria. Kwa kawaida vipingamizi vya kumnyima mshtakiwa dhamana hutolewa na waendesha mashtaka wa serikali na mara nyingi vipingamizi hivyo hutolewa mara tu mshtakiwa anapoomba dhamana. Vipingamizi vya kumkatalia mshtakiwa asipewe dhamana havina budi kuwekwa kabra mshtakiwa hajapata dhamana, kama akishapewa dhamana hivyo havitakuwa vizuizi tena ila huweza kutumika kama sababu za maombi ya kufuta dhamana iliyowekwa.

5.1. Vipingamizi vya Dhamana

Vipingamizi dhidi ya maombi ya dhamana vyaweza kuwa kimoja kati ya vifuavyo, baadhi yake au hata vyote kwa pamoja:

- a. Kama mshtakiwa ataachiwa kwa

dhamana, ataingilia na kuharibu ushahidi na pia atavuruga uchunguzi wa polisi kwenye kesi;

- b. Kama mshtakiwa ataachiwa kwa dhamana atafanya kosa kama lile aliloshtakiwa nalo au kosa jingine lolote la jinai;
- c. Mshtakiwa siyo raia wa nchi hii na ana vitu vyenye thamani katika nchi nyingine;
- d. Mshtakiwa anaishi mpakani karibu sana na nchi jirani na kwamba akipewa dhamana anaweza kutoroka na kuingia nchi nyingine;
- e. Mshtakiwa hana sehemu maalum ya kuishi;
- f. Uzito wa kosa analoshtakiwa mshtakiwa; iwapo kosa analoshtakiwa mshtakiwa ni zito kama vile mauaji, wizi wa kutumia silaha, kupatikana na madawa ya kulevyta, utakatishaji wa fedha na uhaini na iwapo alitiwa hatiani na adhabu kali ikatolewa, ni rahisi kwa mshtakiwa kushawishika kutoroka.

KUMBUKA:

Ni wajibu wa Mahakama kuhakikisha kwamba dhamana inatolewa kwa kufuata haki na kwamba misingi iliyowekwa na sheria haikiukwi kwani dhamana ni haki ya kikatiba.

5.7. Masharti ya Dhamana

Ili mshtakiwa apewe dhamana ni lazima awe na mdhamini au wadhamini. Mdhamini ni mtu mbali na mshtakiwa ambaye hukubaliana na Mahakama husika kwamba endapo mshtakiwa hatafika mahakamani kujibu mashtaka alivyopangiwa na Mahakama, atawajibika kutekeleza masharti aliyoahidi kwenye maombi ya dhamana kama ilivyopangwa na Mahakama. Aidha, mdhamini huihakikishia Mahakama kwamba atasaidia katika kutimiza azma ya kumfikisha mshtakiwa mahakamani kujibu shtaka lake.

Endapo mtuhumiwa hatafika kujibu shtaka kama ilivyokubaliwa, basi

mdhamini atawajibika kulingana na masharti yaliyokuwa katika dhamana iliyotolewa. Vilevile, mpewa dhamana (mshtakiwa) hutakiwa kusaini hati maalum ya kuonyesha atatii masharti yote ya dhamana.

Hati hii ya utiifu hueleza kwamba endapo mshtakiwa hatafika mahakamani kujibu shtaka kama ilivyopangwa, atawajibika kulipa kiwango fulani cha fedha mahakamani. Kwa hiyo mdhamini hujifunga kwa kuihakikishia mahakama husika kuwa mshtakiwa atafika kujibu shtaka kama itakavyopangwa na Mahakama.

Zingatia:

Siyo kila mtu anaweza kumdhamini mtu hivyo lazima yafuatayo yazingatiwe:

- i. Mwenye kumdhamini mshtakiwa lazima awe ni mtu wa kuaminika;
- ii. Uwezo wa Mahakama kutoa dhamana

- umewekwa na sheria kwa hiyo mahakama haina budi kuzingatia misingi ya sheria katika kutekeleza wajibu wake kuhusiana na dhamana;
- iii. Mahakama inapaswa kuhakikisha kwamba misingi ya haki na kanuni za sheria ya jinai hazikiukwi katika kutoa au kukataa kutoa dhamana.

Ikumbukwe:

Isipokuwa pale sheria inapotamka vinginevyo, dhamana ni haki ya kikatiba ya mtuhumiwa kwa utaratibu uliowekwa na sheria kwa hiyo mtuhumiwa ana haki ya kuomba dhamana wakati wowote kabla hajapatikana na hatia.



Norwegian Embassy



Ministry for Foreign
Affairs of Finland

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU (MAKAO MAKUU)

Jengo la Jaji Lugakingira,

S. L. P. 75254, Kijitonyama, Dar es Salaam - Tanzania

Simu: +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037

Barua Pepe: lhrc@humanrights.or.tz

Tovuti: www.humanrights.or.tz

KITUO CHA MSAADA WA SHERIA

Mtaa wa Isere - Kinondoni, S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania

Simu/Nukushi: +255 22 2761205/6

Barua Pepe: legalaid@humanrights.or.tz

OFISI YA ARUSHA

Barabara ya Olerian, Olosiva, Kitalu Na. 116/5, Sakina kwa Idd,

S. L. P. 15243, Arusha – Tanzania **Simu:** +255 27 2544187

Barua Pepe: lhrcarusha@humanrights.or.tz

OFISI YA DODOMA

Kitalu na 22. Area D, S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania

Simu/Nukushi: +255 262350050

Barua pepe: lhrc@humanrights.or.tz

